



## Tathmini za Ujuzi Bure na za Kufuatiliwa kwa haraka

Ikiwa wewe ni mhamiaji anayeishi Australia, unaweza kustahiki kushiriki katika Jaribo la Fursa za Tathmini ya Ujuzi kwa Wahamiaji.

### Je, ni ofa gani iliyopo?

Tathmini za ujuzi bure na za kufuatiliwa haraka kwa wahamiaji nchini Australia walio na ujuzi, sifa, au uzoefu katika kazi zinazohitajika sana.

### Tathmini ya ujuzi inaweza kukusaidia kupata kazi unayotaka

Tathmini ya ujuzi inatathmini ujuzi wako, sifa na uzoefu wa kazi.

### Matokeo ya mafanikio yanamaanisha kuwa ujuzi wako unatambuliwa nchini Australia.

### Ruka foleni - tathmini ya ujuzi wako ikamilike haraka

Baada ya kutoa hati zote zinazohitajika, utapokea matokeo ya tathmini yako ya ujuzi wako katika takriban siku 15 za kazi.

### Unaweza kustahiki ikiwa:

- ✓ una ujuzi, uzoefu na/au sifa katika taaluma inayostahiki
- ✓ bado hujapata tathmini ya ujuzi iliyokamilishwa katika kazi uliyochagua
- ✓ unaishi nchini Australia kwa viza inayostahiki ya familia, mwenzi, mkimbizi au viza ya kibinadamu, na visa yako ilitolewa mnamo au baada 1 Januari 2016.

### Kutuma ombi la Majaribio haya:

Wasiliana na Mamlaka ya Kutathmini kazi inayofaa zaidi kwa ujuzi wako, sifa, au uzoefu.

Mamlaka za Kutathmini zina jukumu la kufanya tathmini za ujuzi na kuna Mamlaka tofauti za Tathmini kwa kazi tofauti.

Mamlaka yako ya Kutathmini itaangalia kama unastahiki.

Fanya haraka kwa sababu hii ni fursa yenye mpaka - **TUMA OMBI LEO!**

### Kwa habari zaidi:

Tembelea tovuti ya Majaribio ya Tathmini ya Ujuzi:

[www.dewr.gov.au/skills-assessment-pilots](http://www.dewr.gov.au/skills-assessment-pilots)

Jua zaidi!

